# MITUME WA QURAN: UTANGULIZI (SEHEMU YA 2 KATI YA 2)

**Ukadiriaji:**

**Maelezo:** Kuwaamini manabii wa Mungu ni sehemu muhimi ya imani ya Kiislamu. Sehemu ya 2 itataja manabii wote waliokuja kabla ya Mtume Muhammad, amani iwe juu yake, waliotajwa katika maandiko ya Kiislamu kuanzia Lutu hadi Yesu.

**Aina:** Makala Imani za Uislamu Hadithi za Mitume

**Na:** Imam Mufti (© 2013 IslamReligion.com)
**Iliyochapishwa mnamo:** 10 Dec 2021
**Ilirekebishwa mara ya mwisho mnamo:** 18 Nov 2021



9. Luti au *Loot* ametajwa mara 17 katika Qurani. Yeye ni mpwa wa Ibrahimu, mwana wa nduguye Ibrahimu. Luti aliishi kwa ncha ya kusini ya Bahari ya Chumvi. Watu wake walikuwa wa Sodoma na Gomora. Luti alimwamini Ibrahimu na baada ya kurudi kutoka Misri, wakaishi kwa maeneo tofauti. Watu wa Sodoma walikuwa wa kwanza kufanya ushoga. Ndiyo sababu mashoga wakati mwingine huitwa wasodoma. Mke wake hakuwa Muumini. Yeye hakufanya dhambi hiyo, lakini aliikubali. Mawe yalinyesha kama mvua juu ya watu wa Sodoma na Gomora na yaliwaangamiza.

10. *Yaqub* au Yakobo, mwana wa Isaka na mjukuu wa Ibrahimu anatajwa mara 16 katika Qurani. Jina jingine la Yakobo lilikuwa Israeli. "*Bani Israel*," Wana wa Israeli, au Waisraeli walipewa jina hilo kwa sababu yake. Manabii wote wa Kiebrania walitoka kwake, na wa mwisho kati yao alikuwa *Eesa* au Yesu. Yakobo ni baba wa makabila kumi na mawili yaliyojulikana kama *Al-Asbaat* (7:160) katika Qurani. Inasemekana alisafiri kuenda kaskazini mwa Iraki, akarudi Palestina na kisha kukaa Misri na kufa hapo. Alizikwa Hebroni, Palestina, pamoja na baba yake kulingana na usia wake wa mwisho. Biblia inataja kuwa Isaka alimwoa Rebeka na mwanawe Yakobo alimwoa Raheli (*Rahil* kwa Kiarabu).

11. *Yusuf* au Yosefu, mwana wa Yakobo au Israeli anatajwa mara 17 kwa Qurani. Aliachwa katika kisima huko Yerusalemu na ndugu zake, halafu akapelekwa Misri ambapo alipata cheo cha juu kwa serikali. Baadaye, baba yake, Yakobo, na ndugu zake walikaa Misri.

12. *Shuaib* au Yethro, aliyetajwa mara 11 katika Qurani, alitumwa kwa watu wa *Madyan*, na alikuwa mmoja kati ya wana wa Ibrahimu. *Shuaib* aliishi kati ya wakati wa Lutu na Musa na alikuwa nabii Mwarabu. Watu wake waliabudu mti uitwao *Al-Ayka* (15:78, 26:176, 38:13, 50:14). Walikuwa wakiwapora watu barabarani, na kuwalaghai katika shughuli za biashara. Basi zikawashukia adhabu kadhaa: Kilio cha kutisha kilichokuwa na tetemeko la ardhi kiliwaangamiza.

13. *Ayyub* au Ayubu ametajwa mara 4 katika Qurani. Inasemekana aliishi karibu na Bahari ya Chumvi au Dameski. Alikuwa nabii mwenye utajiri aliyetahiniwa na Mungu kwa ufukara na ugonjwa, lakini alikuwa na subira na alisaidiwa na mke wake mwaminifu ambaye alikaa naye kwa kila shida. Hatimaye, Mwenyezi Mungu anawalipa vizuri kwa uvumilivu wao.

14. *Yunus* au Yona, pia anajulikana kama "*Dhun-Noon*," anatajwa mara 4 katika Qurani. Aliishi Ninawi, karibu na Mosul, nchini Iraki. Aliwaacha watu wake kabla Mungu hajampa ruhusa, akaeleka nchi ambayo kwa sasa inajulikana kama Tunisia, lakini aliishia Yafa. Alimezwa na nyangumi, kisha akamtubia Mungu na kurudi kwa watu wake huko Iraki ambapo wote, wakiwa na idadi ya 100,000 walitubu na kumwamini.

15. *Dhul-Kifl* ametajwa mara mbili katika Qur'ani. Baadhi ya wasomi wanasema alikuwa mwana wa Ayubu, wengine wanasema yeye ndiye Ezekieli wa Biblia.

16. *Muusa* au Musa ndiye nabii aliyetajwa mara nyingi katika Qurani, akitajwa mara 136. Kabla ya Musa, Yosefu alikuwa ameanza kueneza ujumbe wa umoja wa Mungu (*tawhid*: ibada ya Mungu Mmoja, Mungu wa kweli) miongoni mwa watu wa Misri. Ujumbe wake uliimarishwa wakati baba yake, Yakobo, na ndugu zake pia walikuja kukaa Misri, wakiwabadilisha polepole watu wa Misri nzima. Baada ya *Yusuf*, Wamisri waligeuka tena kwa ushirikina (*shirk*) na watoto wa Yakobo, Waisraeli, wakaongezeka na kupata umaarufu kwa jamii. Musa alikuwa nabii wa kwanza aliyetumwa kwa Waisraeli wakati Farao wa Misri alikuwa akiwafanya watumwa wake. Musa alikimbilia *Madyan* ili kuepukana na mateso. Mungu alimfanya nabii huko Mlima *Toor*, ulio katika Sinai na alipewa miujiza tisa kubwa.

17. *Haroon* au Haruni ni ndugu wa Musa na anatajwa mara 20 katika Qurani.

18,19. *Ilyas* au Eliya na *Yas'a* wanatajwa wote mara mbili katika Qurani. Wote wawili waliishi Baalbek.

20,21. *Dawud* au Daudi anatajwa katika Qurani mara 16. Aliwaongoza Waisraeli kwenye vita na kushinda, na alikuwa na miujiza mingi. Mwanawe, *Suleiman* au Sulemani anatajwa mara 17 na pia alikuwa mfalme mwenye miujiza mikubwa. Wote wamezikwa Yerusalemu.

22. *Zakariyyah* au Zekaria anatajwa mara 7. Alikuwa seremala. Alimlea Maria, mama yake Yesu.

23. *Yahya* au Yohana ni mwana wa Zekaria na anatajwa mara 5. Aliuawa Yerusalemu, na kichwa chake kikapelekwa Dameski.

24. Jina la *Eesa* au Yesu limetajwa mara 25, Masihi mara 11, na 'mwana wa Maryamu' mara 23. Alizaliwa Bethlehemu, Palestina. Inasemekana alitembelea Misri akiwa na mama yake. Yeye ndiye nabii wa mwisho miongoni mwa Wana wa Israeli.

Manabii watano walikuwa Waarabu: *Hud*, *Salih*, *Shuaib*, *Ismail*, na Muhammad, amani iwe juu yao. Wanne kati yao walitumwa kwa Waarabu, na Muhammad alitumwa kwa wanadamu wote.

Kwa kumalizia, manabii, wa biblia na wasio wa Biblia, ni watu wenye umuhimu mkubwa katika maandiko ya Kiislamu. Waislamu wanajiona kama warithi wa kweli wa utume wa manabii waliotumwa na Mungu kwa ubinadamu: ibada ya Mungu Mmoja wa Kweli na utiifu Kwake.

Marejeleo yaliyochaguliwa:


1. Ibn Kathir. *Qasas ul-Ambiya*. Cairo: Dar at-Taba'a wa-Nashr al-Islamiyya, 1997.

2. Ibn Hajr al-Asqalani. *Tuhfa ul-Nubala' min Qasas il-Ambiya lil Imam al-Hafid Ibn Kathir*. Jedda: Maktaba as-Sahaba, 1998.

3. Mahmud al-Masri. *Qasas ul-Ambiya lil-Atfaal*. Cairo: Maktaba as-Safa, 2009.

4. Dr. Shawqi Abu Khalil. *Atlas al-Quran*. Damascus: Dar-ul-Fikr, 2003.



Anwani ya wavuti ya makala hii:

https://webcache001.islamreligion.com/sw/articles/10233/mitume-wa-quran

Hakimiliki © 2006-2020 Haki zote zimehifadhiwa. © 2006 - 2026 IslamReligion.com. Haki zote zimehifadhiwa.